**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA KILIMO**

**SHIRIKA LA UKAGUZI NA USIMAMIZI WA VYAMA VYA USHIRIKA (COASCO)**

*Unapojibu tafadhali taja:*

**Kumb. Na. CA.61/287/01/4** **03.04.2025**

Wenyeviti na Wajumbe wa Bodi,
Vyama vya Ushirika,
**TANZANIA BARA**

**YAH: MWALIKO WA MAFUNZO YA SIKU TATU KWA WATENDAJI NA VIONGOZI WA VYAMA VYA USHIRIKA KUHUSU MASUALA YA UHASIBU NA KODI KATIKA UKUMBI WA MABEYO JIJINI DODOMA KUANZIA TAREHE 23 HADI 25 APRIL, 2025**

Husika na Kichwa cha Habari hapo juu.

2. Moja ya jukumu la COASCO kama ilivyoainishwa kwenye Kifungu Na 4 (1) (b) na (d) cha Sheria Na. 15 ya Ukaguzi na Usimamizi wa Vyama vya Ushirika ya mwaka 1982 iliyorekebishwa mwaka 2005 ni kutoa Ushauri na mafunzo kwa Vyama vya Ushirika ili kuvijengea uwezo wa kiutendaji, usimamizi wa rasilimali na uandaaji wa taarifa za fedha unaozingatia viwango vya uhasibu vya kimataifa.

3. Hivyo, **COASCO** imeandaa program ya mafunzo maalum kwa vitendo ya muda wa siku tatu kuhusu masuala ya Uhasibu na Kodi. Mafunzo hayo yatatolewa kwa **Watendaji ambao ni Meneja, Mhasibu mkuu, Wahasibu wasaidizi, Mkaguzi mkuu wa ndani na Wajumbe wa Bodi** na mtu yoyote ambaye atapenda kupata ujuzi kwenye hayo; na yatafanyika katika ukumbi wa JENERALI MABEYO jijini Dodoma tarehe 23 hadi 25 April, 2025 kuanzia saa mbili kamili asubuhi.

4. Kila mshiriki anatakiwa kuchangia ada ya Tshs 350,000 ambayo inajumuisha gharama ya mafunzo ya siku tatu, ukumbi, chai na chakula cha mchana wakati wa mafunzo. **Malipo hayo yatalipwa kupitia nambari ya malipo ya Serikali** itakayotolewa baada ya kuthibitisha ushiriki wako kwa kuwasiliana na RCA au mratibu wa mfunzo (CPA Gabriel Msuya) kupitia **nambari ya simu 0762 389 616** au barua pepe **gabriel.msuya@coasco.go.tz**

5. Tafadhali unaombwa kuhakikisha uthibitisho wa ushiriki wako kwa wakati na malipo yafanyike mnamo au kabla ya tarehe **22 April, 2025**.

Natanguliza shukrani,

Pamoja tujenge Uchumi.

**CPA Gabriel L. Msuya**
**KNY: MKURUGENZI MKUU**